BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

BARAZA LA KUMI NA MOJA

RATIBA YA MKUTANO WA TANO WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

TAREHE 25 NOVEMBA – 11 DISEMBA, 2026

CHUKWANI 25/11/2026

RATIBA YA MKUTANO WA NNE WA BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI
UTAKAOANZA TAREHE 25 NOVEMBA 11 DISEEMBA, 2026

SIKU NA TAREHE	SHUGHULI
JUMATANO - ALHAMIS *25 – 26 /*11/2026	(i) Maswali na Majibu (ii) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Usalama na Afya Kazini, Nam. 8 ya 2005 na Kutunga Sheria ya Usalama na Afya Kazini kwa ajili ya kuhakikisha usalama, afya na ustawi wa watu kazini na kuwalinda watu wengine dhidi ya hatari zinazotokana na shughuli za kazi na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo.
IJUMAA 27/11/2026	(i) Maswali na Majibu (ii) Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake.
JUMAMOSI & JUMAPILI 28/11/2026 & 29/11/2026	MAPUMZIKO YA MWISHO WA WIKI
JUMATATU 30/11/2026	(i) Maswali na Majibu (ii) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Chuo cha Fedha Zanzibar, Kuweka Masharti ya Utoaji wa Elimu katika Fani za Biashara na Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo
JUMANNE *01/12/2026*	(i) Maswali na Majibu (ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar (ZFDA), 2024/2025 (iii) Ripoti ya Utekelezaji wa kazi za Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI), 2024/2025
JUMATANO 02/12/2026	(i) Maswali ya Papo kwa Papo kwa Mkuu wa Shughuli za Serikali katika Baraza (ii) Maswali na Majibu (iii) Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Shughuli za Maendeleo katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na

	Teknolojia (KIST), 2024/2025 (iv) Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Shughuli za Maendeleo katika Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar (BOHUMAZA), 2024/2025
ALKHAMIS *03/12/2026*	(i) Maswali na Majibu (ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Shughuli za Maendeleo katika Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar, 2024/2025 (iii) Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Shughuli za Maendeleo katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), 2024/2025
IJUMAA 04/12/2026	(i) Maswali na Majibu (ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Wakala wa Barabara Zanzibar (ZANROADS), 2024/2025
JUMAMOSI & JUMAPILI 05/12/2026 & 06/12/2026	MAPUMZIKO YA MWISHO WA WIKI
JUMATATU 07/12/2026	(i) Maswali na Majibu (ii) Taarifa ya Utendaji Kazi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), 2024/2025 (iii) Taarifa ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), 2024/2025 (iv) Ripoti ya Shughuli na Uendeshaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA), 2024/2025
JUMANNE 08/12/2026	(i) Maswali na Majibu (ii) Ripoti ya Hali ya Utumishi wa Umma ya Kamisheni ya Utumishi wa Umma, Zanzibar, 2024/2025 (iii) Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Kazi za Afisi ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar (BLW), 2024/2025
JUMATANO 09/12/2026	(i) Maswali ya Papo kwa Papo kwa Mkuu wa Shughuli za Serikali katika Baraza (ii) Maswali na Majibu (iii) Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), 2024/2025

	(iv) Taarifa ya Utekelezaji wa Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA), 2024/2025
ALKHAMIS 10/12/2026	(i) Maswali na Majibu (ii) Ripoti ya Utekelezaji wa Mwaka ya Tume ya Utangazaji Zanzibar (TUZ), 2024/2025 (iii) Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ), 2024/2025 (iv) Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS), 2024/2025
IJUMAA 11/12/2026	(i) Taarifa ya Utekelezaji ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo, 2024/2025 (ii) Miswada Kusomwa Kwa Mara ya kwanza (iii) Mhe. Makamo wa Pili kuliahirisha Baraza

TANBIHI Ndugu Katibu Mkuu, Mazingira ya majadiliano ndani ya Baraza yanaweza kuifanya Ratiba hii isifuatwe kwa ukamilifu. Jambo la Msingi ni kufuata Orodha ya Shughuli za Baraza (Order Paper) ya kila siku.